**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**
**DODOMA**
**Nambari ya Simu:** 0738 166 703
0733 005 974
**Barua pepe:** secretary@psc.go.tz
***Tovuti:*** *www.psc.go.tz*

Tume ya Utumishi wa Umma,
Jengo la Chimwaga (UDOM),
Ghorofa ya 2,
S.L.P. 1074,
**40405 DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

Mojawapo ya Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma (PSC), yaliyoainishwa katika Kifungu cha 12(1)(d) na Kifungu cha 27(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 (Marejeo ya mwaka 2023), ni Kupokea na Kushughulikia Rufaa na Malalamiko ya Watumishi wa Umma ambao hawajaridhika na Uamuzi uliotolewa na Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma.

Kupitia Taarifa hii, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kufanya Mkutano wa pili kwa mwaka wa fedha 2025/2026, katika Manispaa ya Mji wa Morogoro kuanzia tarehe1/12/2025 hadi tarehe 19/12/2025 katika Ukumbi uliopo Kituo Jumuishi cha Masuala ya Sheria - Morogoro. Katika Mkutano huu Tume itajadili na kutoa Uamuzi wa Rufaa na Malalamiko mbali mbali yaliyowasilishwa na Watumishi wa Umma ambao hawakuridhika na Uamuzi uliotolewa na Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka zao za Nidhamu.

Aidha, katika Mkutano huu, Tume itatoa nafasi kwa Warufani na Warufaniwa walioomba kufika mbele yake na kutoa ufafanuzi wa ziada kuhusu hoja zao za Rufaa mbele ya Tume. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022.

Aidha, Taarifa mbali mbali za Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2025/2026 zitawasilishwa, kujadiliwa na kutolewa maelekezo kwenye Mkutano huu.

Imetolewa na :-

John C. Mbisso
Kaimu Katibu
**TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

28/11/2025